

“Je, Vita Ni Matokeo Ya Dini?”

Umewahi kuwasikia watu wakidai kuwa “vita vyote vinaanzishwa na dini”? Bila dini kusingekuwepo vita.” Karibu kila siku, naona wapagani au watu wengine wakiropoka utumbo huu. Kwamba dini ndiyo sababu kubwa ya vita. Kinachotokea ni kwamba wale wanaomchukia Kristo wanaposikia upuuzi huu wanaona wameungwa mkono. Kisha wanaanza kuruudia na kusadiki uongo kama huo na kuanza kuutumia uongo kwa ajili ya kuhalalisha mtazamo wao kwamba tunatakiwa kujiepusha na ulimwengu wa dini.

Huu ni uozo wa kimtazamo waziwazi ambao umekuwa ukirudiwa siku hizi na baadhi yao kwenye vyombo vyta habari, kama vile, Waliberali wa mlengo wa kushoto, wapagani na watetezi wa haki za wanadamu. Tena wapo wale wenye ajenda na hoja ndogo. Wanapokosa hoja hawaoni shida kuupika uongo ili kusaidia hoja yao.

Kwa kadri ya “Encyclopedia of wars,” iliyoandikwa na Charless Philipps na Alan Axelrod, iliyochapwa mnamo 2004. Wanadamu wamepigana vita 1,763. Kati ya hizo, vita 123 ziliangukia katika uhalali wa kuitwa vita vya kidini. Hii ina maana kuwa 6.8% ya vita vyote vilikuwa ni vya kidini. Vita 66 kati ya 123 vilikuwa ni vita vilivyotokana na Uislam. Vita 57 vilivyobakia vilitokana na mifumo ya kiimani mbalimbali. Kisha mtu anapotazama jumla ya watu waliouawa vitani, 2% ya watu waliouawa waliuawa katika “vita vya kidini”

Pamoja na kusema haya yote, tusinaswe na ulaghai huu. Biblia iko wazi kwamba shetani ni mwongo tangu mwanzo na anaeneza uongo ili kuwazuia watu kwenda kwa Mungu (Yohana 8:44; 1 Timotheo 4:1ff). Moja ya uongo wake mpya kabisa ili kuwazuia watu kwenda kwa Kristo, ni ule kwamba dini ya Kikristo ndiyo chanzo cha vita vyote, na kama si vyote basi vita vingi vimesababishwa na Ukristo.

Pili, tuzingatia kwamba ni dhambi kuwa Ukristo ni kisababishi cha kila vita. Kila vita ilianza aidha kwa; husuda, wivu, magomvi, choyo, chuki, mafundisho ya uongo, dini ya uongo au tama ya madaraka. DHAMBI! Tafadhali, zingatia Marko 7:21-23; Wagalatia 5:19; Yakobo 4:2.

Tatu, Kama kanisa la Bwana, elewa kwamba kati ya vita 1,763 hakuna hata moja iliyosababishwa au kuanzia na Kanisa la Kristo. Agano Jipyä linatufundisha kuwa tunatakiwa kubeba silaha ili kuulinda ufalme wa Mungu au kulitumia jeshi kueneza ufalme wa Mungu duniani leo. Hicho ndicho kinachostaa jabisha kuhusiana na ufalme wa Mungu. Ufalme huu umekuwapo hapa kwa zaidi ya miaka 2,000 bila hata kurusha risasi, na bado twasimama! Ingawaje wapo wengine ambao wameanzisha vita kwa mwamvuli wa “Jina la Yesu” hata wakafanya mambo ya kutisha duniani. Lakini hawakufanya hivyo kwa mamlaka wala ruhusa ya Yesu. Katika kila kisa, ni mafundisho ya uongo yaliyopelekea mapigano. Kanisa la Bwana la kweli, ambalo ni kanisa la Agano Jipyä, halijawahi kuanzisha vita ya kimwili. Hakuna kibali cha vita kama hiyo kwenye maandiko. Hakujawahi kuwapo sababu hasa kwa kuwa Mungu ndiye...”ukuta wa moto, kuuzunguka pande zote, nami nitakuwa huo utukufu ndani yake,” Zecharia 2:4-5

